

# HALAMASHAURI YA MJI MAFINGA

SHULE YA SEKONDARI  
ISALAVANU

S.L.P 56

**MAFINGA**

**14/12/2020**

KUMB NA.HM/MAF/2020/03

.....

.....

S L P.....

**MAFINGA**

## **YAH:MAAGIZO YA MWANAFUNZI ALIYECHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI ISALAVANU MWAKA 2021**

Ninayo furaha kukupa taarifa ya kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari isalavanu mwaka 2021

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 saa moja kamili asubuhi.

Tunaamini wakati wote utakaokuwa Isalavanu sekondari utakuwa tayari kupokea,kujifunza,kutii na kutekeleza maagizo,kufuata sheria na taratibu za shule

Shule ya sekondari isalavanu ni ya kutwa kwa wavulana na tunayo nafasi ya hosteli kwa wasichana na ili mwanao wa kike aweze kusoma vizuri tunashauri mzazi kuona umhimu wa kumleta mwanao Hosteli.

### **MAHITAJI KWA WANAFUNZI WOTE WAVULANA NA WASICHANA**

1. Mashati/Blauzi nyeupe mikono mirefu aina ya tetroni mawili (2)
2. Soksi ndefu nyeusi jozi (2) kwa wavulana na soksi ndefu nyeupe jozi mbili (2) kwa wasichana.
3. Viatu vya ngozi nyeusi vyenye kamba na vyenye visigino vifupi jozi mbili (2)
4. Suruali mbili (2) kwa wavulana na ishonwe mshono wa heshima siyo ya kubana chini na iwe na mfuko mmoja nyuma siyo miwili na sketi mbili (2) kwa wasichana zenye marinda madogomadogo na iwe ndefu kuvuka magoti kwenda chini rangi ya udongo pamoja na tai ndefu Rangi ya udongo kwa wavulana na wasichana.
5. Sare zote ziwe mpya na mwanafunzi hatapokelewa kwa kuvaa sare iliyokwisha kutumika
6. Kwa wasichana waislamu watashona hijabu na suruali ya heshima ambayo rangi yake ifanane na rangi ya udongo kama ilivyoelekezwa hapo juu

7. Nguo za michezo ni trakisuti nyeusi yenye mistari miupe kwa wavulana na wasichana pamoja na raba za michezo na T-sheti ya dark bluu ambayo itapatikana shuleni na zitavaliwa siku ya michezo kwa wanafunzi wote.

8. Sweta jozi mbili (2) Rangi ya zambarau kwa wanafunzi wote

9. Daftari kubwa (counter books) zisipungue 10 na kalamu za wino wa bluu au mweusi,penseli,rula ,mkebe (mathematical seti) mmoja (1).

10. Cheti cha kuzaliwa chenye jina linalofanana na jina ulilofanyia mtihani wa darasa la saba,uje na kopi yake siku ya kuripoti shuleni,hapa shuleni tunatoa huduma ya kopi kwa hiyo unaweza kuja kupata huduma hii hapa shuleni.

11. Kwa wasichana wanaotaka kukaa hosteli washonewe gauni la dark bluu ambalo litakuwa linavaliwa wakati wa kazi za nje .(shamba dress)

12 .Mwanafunzi aje na picha mbili (2) za ‘‘passport size’’ zenye rangi ya bluu

13. Mwanafunzi aje na kifaa cha usafi ambacho ni jembe na chelewa.Pia mwanafunzi anapokuja kuripoti aje na mzazi au mlezi wake kama hana mzazi na si vinginevyo.

Mwanafunzi anatakiwa kukamilisha fomu zifuatazo kabla ya kuja shuleni na aje nazo zikiwa zimejazwa kwa ukamilifu.

1. Fomu ya maelezo ya daktari kuhusu afya ya mwanafunzi (medical certification)

2 .Fomu ya kukubali nafasi uliyopewa kujiunga na shule ya sekondari isalavanu.

Mwanafunzi atapokelewa tu kwa kukamilisha maagizo yote hapo juu na tunaomba wazazi wawe wazi kwa mwanafunzi mwenye matatizo ili tujue namna ya kumsaidia kama vile afya,nidhamu. n.k

**NB:Wazazi/walezi wote wahakikishe wanafunzi wanaripoti ndani ya wiki ya kwanza baada ya kufungua shule ili aweze kuanza vizuri masomo ya kujifunza kingereza**

**SHULE ITAFUNGULIWA TAREHE 11/01/2021 SAA 1:00 ASUBUHI.**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI ISALAVANU: ELIMU NI UFUNGUO WA MAENDELEO (EDUCATION IS A KEY TO DEVELOPMENT) FANYA BIDII KATIKA KUSOMA.**

.....

**GEREMIA C. LALIKA**

**MKUU WA SHULE**